**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
**DODOMA**

*Simu:* +255 026 23222761-5
*Fax No.* +255 026 2322624
**E-mail:** cna@bunge.go.tz

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Vikao vya Kamati 14 za Kudumu za Bunge vitaanza Jumatatu tarehe 21 Oktoba na kuendelea hadi tarehe 01 Novemba 2019, Jijini Dodoma. Shughuli zote za Kamati katika kipindi hicho zimepangwa kwa kuzingatia Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. Shughuli hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kupokea na kujadili Taarifa ya Mapendekezo ya Mwongozo wa kutayarisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

(ii) Uchambuzi wa Taarifa ya Msajili wa Hazina kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma katika Mashirika na Taasisi mbalimbali Nchini.

(iii) Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Serikali za Mitaa na za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Juni, 2018.

(iv) Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali.

(v) Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Kumi na Sita wa Bunge.

Ratiba zote za Shughuli za Kamati za Bunge zinapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni www.parliament.go.tz.

**Imetolewa na:** Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa
Ofisi ya Bunge
**DODOMA**

16 Oktoba, 2019